Tovuti:www.nsimbodc.go.tz

# Nsimbo Wiki hii

*Jarida Mtandao la Wiki la Halmashauri*

TOLEO NAMBA 01

NOVEMBA 09,2018

## Msimu wa Kilimo 2018 wazinduliwa rasmi Nsimbo,

- *Maafisa Ugani Kata/Vijiji hakuna kulala,*
- *Wakulima kupewa "Maujanja"kuleta tija uzalishaji,*
- *Wasisitizwa Mazao ya biashara kuchochea ukuaji Uchumi wa Viwanda*



*Pichani :Mgeni Rasmi katika Uzinduzi wa Msimu wa Kilimo 2018,Mkuu wa Wilaya ya Mpanda Mh.Lilian Charles Matinga akizungumza na Wakulima katika Shughuli ya uzinduzi wa Msimu wa Kilimo 2018 katika Eneo la Kanoge Centre katika Kata ya Kaoge Nsimbo.*

*Na :John Mganga*

Wakulima Wilayani Mpanda Mkoani Katavi wametakiwa kuachana na Kilimo cha mazoea na badala yake kutumia vema Elimu ya Kilimo inayotolewa na **Maafisa kilimo wa Halmashauri,Maafisa Ugani katika ngazi ya Vijiji na Kata pamoja na Wadau mbalimbali wa Kilimo wakiwemo Wasambazaji wa pembejeo za Kilimo Nchini** ili kuhakikisha kuwa Wanatumia ipasavyo elimu ya mbinu bora za kilimo kuleta tija katika uzalishaji Mazao kwa Msimu wa Kilimo 2018……………..Uk 2

## *Wafugaji Nyuki Nsimbo wapatiwa Mafunzo Ufugaji wa Kisasa*

*Na:John Mganga*

Uzalishaji wa mazao yatokanayo na ufugaji Nyuki Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo unatarajiwa kuongezeka maradufu kutokana na Wafugaji nyuki kupewa mafunzo ya Ufugaji wa nyuki kwa njia za kisasa na za kitaalamu.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.Said Mpumbi** katika Mafunzo ya Ufugaji wa Nyuki kisasa yaliyofanyika Novemba 8,2018 katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo yakihusisha wafugaji Nyuki wa Kata za Kapalala Uruwila na Mtapenda…………..Uk 3

*Jarida Mtandao la kila Wiki la Nsimbo Wiki Hii limeandaliwa na Kitengo cha Teknolojia ya Habari,Mawasiliano na Uhusiano Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.*

*Wasiliana nasi kupitia Barua pepe ,info@nsimbodc.go.tz,Tembelea tovuti yetu www.nsimbodc.go.tz.*

## Uzinduzi Msimu wa Kilimo 2018…….inatoka Uk. wa kwanza

Akizungumza na Wakulima katika uzinduzi huo Novemba 9.2018,**Bi Matinga** amebainisha kuwa kutofanya maandalizi kwa wakati katika misimu ya Kilimo kumekuwa sababu kubwa inayoathiri kwa kiasi kikubwa ustawi wa mazao na hivyo kuathiri uzalishaji wa Mazao Mashambani jambo linalopelekea kushuka kwa kiwango cha Mavuno.

Kutokana na changamoto hiyo, **Bi Matinga** amewataka Maafisa Ugani ngazi ya Vijiji na Kata Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kuhakikisha kuwa washirikiana na Wakulima kwa karibu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanatoa ushauri wa Kitaalamu kwa Wakulima ili kuhakikisha kuwa Wakulima wanatumia mbinu bora na za kisasa kwa msimu huu wa Kilimo 2018 ili kuongeza tija katika Uzalishaji.

Amesema Serikali inatambua changamoto ya Uhaba wa Maafisa Ugani na kwamba hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Halmashauri ili kuhakikisha kuwa inaondokana na Changamoto hiyo inayoathiri kwa kiasi kikubwa Sekta ya Kilimo Nsimbo.

Awali Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Mh.Raphael Kalinga** akizungumza katika uzinduzi huo amesisitiza juu ya umuhimu wa Wakulima Nsimbo kulima Mazao kulingana na mahitaji ya soko kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuuza mazao kwa wakati na hivyo kunufaika na Kilimo.

**Mwenyekiti Kalinga** ametoa wito kwa wakulima Nsimbo kuhakikisha kuwa wanalima mazao ya biashara hususani Pamba kwa kuwa zao hilo limethibitika kustawi vizuri Mkoani Katavi na kwamba kwa Msimu wa Kilimo uliopita Pamba kutoka Katavi imethibitika kua na ubora na Viwango vya kuridhisha.



*Pichani:Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Mh.Raphael Kalinga(Mwenye shati Jeupe) akizungumza na Wakulima wa Kanoge katika shughuli ya Uzinduzi wa Msimu wa Kilimo 2018 Nsimbo.(Picha na John Mganga)*

**Aidha Mh.Kalinga** amesema endapo wakulima Nsimbo watatumia vema fursa ya kulima mazao ya biashara itasaidia kwa sehemu kubwa ongezeko la malighafi jambo litakalochochea ujenzi wa Viwanda Mkoani Katavi jambo litakalopelekea Wananchi hao kunufaika na Viwanda hivyo kutokana na kuuza mazao yao ndani ya Mkoa badala ya kusafirisha umbali mrefu kwenda kuuza katika Mioa ya mbali.

Kwa Upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.Mohamed Ramadhani** amesema Dira ya Halmashauri katika Sekta ya Kilimo ni kuhakikisha kuwa Kilimo kinakua na tija kwa wakulima.

Amesema ni muhimu Wakulima katika Msimu huu wa Kilimo kutoa kipaumbele katika uzalishaji wa Mazao ya Biashara sambamba na kuchukua hatua za haraka za kuwasiliana na Maafisa Ugani pamoja na Wadau wa Kilimo kwa ajili ya kupata suluhu pindi dalili za awali za uharibifu wa mazao unapotokea.

Mh.Kalinga amesema endapo wakulima Nsimbo watalima kwa mchanganyiko yaani mazao ya biashara na Mazao ya Chakula itasaidia kuondoa tatizo la Njaa ambalo huwatesa wakulima kutokana na kuzalisha aina moja ya mazao ya chakula na kujikuta wakiuza pasi kuweka akiba ya chakula

Kwa Upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Mohamed Ramadhani a ametoa wito kwa walulima Nsimbo kujiandikisha ili kuweza kutambulika kwa urahisi jambo litakalorairahisishia ofisi yake kuwahudumia kwa urahisi zaidi .

# Wafugaji Nyuki Nsimbo …………….Inatoka Uk…1

**Mpumbi** amebainisha kuwa uzalishaji wa mazao yatokanayo na ufugaji wa Nyuki katika sehemu nyingi Nchini umekuwa ukiathiriwa zaidi kutokana na Wafugaji kutokuwa na elimu na uelewa wa kutosha kuhusu Ufugaji wa Nyuki kwa njia za kisasa na za kitaalamu.

Ameeleza kuwa Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za makusudi kuhakikisha kuwa elimu ya kutosha inatolewa kwa Jamii za Wafugaji wa nyuki ambapo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa mara kadhaa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Taasisi ya Jane Goodal,pamoja na Wakala wa Usimamizi wa Misitu Nchini TFS.

Amesema ni jukumu la Wafugaji Nyuki Nsimbo kuhakikisha kuwa wanatumia ipasavyo Elimu inayotolewa na Halmashauri kupitia kitengo cha Nyuki kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali ili waweze kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya Nyuki Nsimbo na kuondokana na ufugaji wa asili ambao hauna tija.

**Mpumbi** amewaambia washiriki wa Mafunzo ya ufugaji wa Nyuki kuwa jukumu lao pia kuhakikisha kuwa wanazingatia uhifadhi wa mazingira katika shughuli za ufugaji wa nyuki ili kuhakikisha kuwa ufugaji wa Nyuki unaleta Tija katika Utunzaji wa Mazingira.

Akizungumzia kuhusu uzalishaji wa mazao yatokanayo na ufugaji wa Nyuki Nsimbo Mkuu huyo wa Kitengo amesema uzalishaji wa Asali umepungua kutoka takribani lita 102,170 mwaka 2016/2017 hadi kufikia Lita 99,530 mwaka 2017/2018 ambapo kwa zao la Nta uzalishaji umeongezeka kutoka wastani wa Kilo 9195.5 mwaka 2016/2017 hadi Kilo 9336.5 kwa mwaka 2017/2018 ambapo ameeleza kuwa uzalishaji umepungua kutokana na Mabadiliko ya Hali ya Hewa.

Aidha kwa upande wa Mizinga ya kisasa amebainisha mizinga hiyo kuongezeka kutoka Mizinga 4928 mwaka 2016/2017 hadi kufikia Mizinga 8363 kwa mwaka 2017/2018 ambapo kuongezeka huko kumechangiwa zaidi na jitihada za utoaji wa Elimu kwa Wafugaji Nyuki Nsimbo.

Akifunga mafunzo hayo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashari ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Mohamed Ramadhani amewataka Wafugaji hao wa Nyuki kufuga kwa Malengo ili waweze kujikwamua na Umasikini.

Mafunzo hayo ya siku Nne yanayotolewa na **Kitengo cha Nyuki Nsimbo** kwa Kushirikiana na Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu Nchini TFS Mpanda, yalianza kutolewa rasmi Novemba 5,2018 katika Kata ya Ugalla ambapo yatamalizika leo Novemba 8,2018 yakihusisha Kata za Uruwila,Kapalala na Mtapenda za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.



*Pichani:Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Mohamed Ramadhani akizungumza wakati wa ufungaji wa Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Kisasa yaliyofnayika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri Novemba 8 ,2018.(Picha na John Mganga)*

# Matukio ya Wiki katika Picha



*Picha Na.1.**Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo George Magille akisoma Taarifa ya Idara wakati wa Uzinduzi wa Msimu wa Kilimo 2018,shughuli iliyofanyika Kata ya Kanoge Enelo la Kanoge Senta Novemba 9 2018**.(Picha Na:John Mganga)*



***Picha Na.2**.Mkuuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Hamis Mnubi akizungumza na Wajasiriamali Waliopatiwa mafunzo ya namna ya Matumizi ya fedha za Mikopo ya Wajasiriamali inayotolewa na Halmashauri Novemba 9,2018 katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.Wajasiriamali hao wanatarajia kunufaika na Mikopo punde baada ya Taratibu za utoaji Mikopo kukamilika((Picha na John Mganga)*



*Picha Na.3.Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.Said Mpumbi** akifundisha kwa Vitendo namna bora ya Uvunaji asali kwa kutumia mavazi ya Kisasa ya yanayoepusha madhara ya kuumwa na Wadudu Nyuki Novemba 8,2018 katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.Picha (Na.John Mganga)*



*Picha Na.4 .Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Mh.Raphael Kalinga** akitoa neno la ufunguzi katika Mafunzo ya Ujasiriamali kwa Vikundi vya Ujasiriamali yaliyofanyika Novemba 9,2018 katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.Vikund hivyo vinatarajia kunufaika na Mikopo mara baada ya Taratibu za utoaji Mikopo kukamilika.(Picha Na:John Mganga)*



*Picha Na.5.Muonekano Mpya wa Kituo cha Afya Kanoge Baada ya Ujenzi na Ukarabati wa kituo hicho kufanyika.Shughuli hiyo iko katika hatua za Mwisho na Wananchi wataanza kunufaika na huduma Bora Picha (Na.John Mganga)*



*Picha Na.6.Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Mh.Raphael Kalinga** Novemba 9 katika Ukaguzi wa Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kituo cha Afya Kanoge Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo .Ujenzi na Ukarabati wa Kituo hicho uko katika Hatua za Mwisho kukamilika.(Picha na :John Mganga)*